UZALISHAJI ~ MWANANCHI UK 12.



# JKT yaanza kuzalisha vifaranga vya samaki

Sharon Sauwa, Mwananchi
ssauwa@mwananchi.co.tz

**Morogoro.** Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) limeanza la kuzalisha vifaranga wa samaki ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan.

Agizo hilo lililotolewa Aprili 6, mwaka 2021 lililenga JKT kufikia uzalishaji wa vifaranga milioni mbili kwa mwezi.

Rais Samia alitoa agilo alipokuwa anawaapisha makatibu wakuu na watendaji mbalimbali wa taasisi, akiiagiza kuzalishwa kwa wingi vifaranga vya samaki ili watu wengi zaidi waweze kunufaika na fursa ya ufugaji wa samaki inayovutia watu wengi hivi sasa.

Mkuu wa Kikosi cha JKT 837 Chita kilichoko wilayani Kolombero, Luteni Kanali Emmanuel Kukula aliyasema hayo wakati wa ziara ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa katika kikosi hicho na shamba lale la Mngeta Plantation Ltd.

Luteni Kanali Kukula alisema kikosi hicho kimetenga ekari 14 kwa ajili ya ufugaji wa samaki na tayari kimeanza shughuli hiyo.

"Katika eneo hilo yamejengwa matanki 16 kati 27 yanayokusudiwa. Tunatarajі kuzalisha tani 12 za samaki na vifaranga milioni mbili kwa mwezi," alisema.

Alisema wanaendelea na uzalishaji lakini hawajafikia idadi hiyo ya vifaranga kwa mwezi na hivi sasa ujenzi wa matanki ya kutotoreshea vifaranga umefikia asilimia 76.

Waziri Bashungwa alisema wanajadiliana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuona namna watakavyoshirikiana katika mradi huo wa ufugaji wa samaki.

Kuhusu utatuzi wa changamoto, Bashungwa alisema amemweleza Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele kupeleka vipaumbele vya mradi bungeni ili vikajadiliwe wakati wa bajeti.

Meja Jenerali Mabele alisema mafanikio yaliyopatikana hayatokani na nguvu zao wenyewe, bali kitendo cha Rais Samia kutamka kuwa itaongezwa bajeti ili kuhakikisha JKT inafanya vizuri kwenye shughuli zake kimewaongezea hamasa.

Alisema miradi ya skimu ya umwagiliaji na ufugaji wa samaki ni sehemu ya mafanikio pia ya miaka 60 ya JKT.

**27**
Mabwawa ya samaki yanayokusudiwa kujengwa na JKT Kambi ya Chita.

**Milioni 2** Idadi ya vifaranga vya samaki vinavyotarajiwa kuzalishwa na kikosi hicho kwa mwezi.

HABARI LEO UK 15.

# 'Vyakula vya mifugo, binadamu vinavyoingizwa nchini hukaguliwa'

**Na Lucy Ngowi**

WAKALA ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) kwa kushirikiana na mamlaka za serikali, umekuwa ukikagua shehena zinazoingizwa nchini zikiwemo za vyakula vya binadamu na mifugo ili kujua ubora wake.

Mtendaji Mkuu wa TVLA, Dk Stella Bitanyi alisema hayo alipozungumza na HabariLEO hivi karibuni.

Alisema kujua ubora wa vyakula vya mifugo ni miongoni mwa dhima ya wakala huo hivyo kuna maabara ambayo inafanya kazi kitaifa katika eneo hilo.


"Sasa hivi tunaendelea kuimarisha hii maabara tupo kwenye mchakato wa manunuzi ya vifaa mbalimbali ikiwemo kupima sumu kuvu. Sumu kuvu ni tatizo, jinsi ambavyo tunahifadhi hizi nafaka sio nzuri kwa afya wala kwa mifugo," alisema.

Alisema pia ni jukumu lao kuhakiki usalama na ubora wa vyakula vya mifugo nchini kwa kupokea sampuli kutoka kwa wakaguzi, kuzipima na kutoa ushauri.

Vile vile hupokea sampuli kutoka kwa watengenezaji wakubwa wa vyakula vya mifugo kwa kuwa wakala una uwezo wa kupima kiwango cha madini mbalimbali yaliyoko kwenye vyakula vya mifugo, madini kwenye maji, pia ubora wa zile malighafi zinazotumika kuandaa vyakula vya mifugo.

Kwa upande mwingine alielezea majukumu ya wakala huo kuwa ni kufanya uchunguzi, utambuzi wa magonjwa ya wanyama na wadudu wanaosambaza magonjwa hayo, lakini pia kufanya utafiti na kuzalisha chanjo.

"Uzalishaji unatokana na tafiti ni lazima tufanye tafiti ili kujua usalama na uhai, kwamba nitakapomchoma chanjo mnyama ule uwezo wa kutengeneza kinga utaishi ndani yake kwa muda gani, lazima tuvifahamu kabla ya kutoa chanjo," alisema.




Wafanyakazi wanawake wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu wakishiriki kutoa elimu ya afya na jinsia kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mwingilo kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani mwishoni mwa wiki. (Picha kwa hisani ya Barrick).

# Meya Ubungo aishukuru DCB uboreshaji wa elimu

**Na Mwandishi Wetu**

MEYA wa Manispaa ya Ubungo, Jafari Nyaigesha amezitaka taasisi mbalimbali kuiga mfano wa Benki ya DCB katika juhudi zake za uboreshaji wa elimu nchini.

Nyaigesha aliyasema hayo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, wakati akipokea msaada wa madawati 30 kwa ajili ya Shule ya Msingi Kiluvya, iliyoko katika Manispaa hiyo jijini Dar es Salaam yakitolewa na DCB kupitia kampeni yake ya 'Elimu Mpango Mzima na Mama Samia'.

"Kwa kufanya hivi, Benki ya DCB inaunga mkono juhudi za Rais wetu Mpendwa, Samia Suluhu Hassan za kuwaletea watu wake maendeleo katika uboreshaji wa elimu nchini," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa DCB, Isidori Msaki akizungumza mahali hapo alisema madawati hayo ni sehemu ya madawati 150 yeye thamani ya Sh milioni 37.5 wanayoyatoa katika Manispaa tano za jiji la Dar es Salaam ikizingatiwa kuwa wao ndio wanahisa waanzilishi wakati benki ikianzishwa miaka 20 iliyopita.

"Tunajivunia ushirikiano wenye tija na Manispaa hizi kwani kwa kipindi cha miaka 20 kwa mtaji wa Sh bilioni 1.7 tuliokuwa nao mwaka 2002, benki imeendelea kukua mwaka hadi mwaka na imeweza kutoa gawio la jumla ya Sh bilioni 11.5 na kati ya hizo, Manispaa zimepokea gawio la Sh bilioni 4.55", alisema Msaki.

Mkurugenzi huyo alisema, mafanikio hayo yamewezekana chini ya uongozi mahiri wa bodi ya benki hiyo inaoongozwa na Zawadia Nanyaro.

CamScanner